## Kusoma Zaidi

# Vipengele vya kuzingatia katika kusoma kwa ufasaha.

- **Kasi ifaayo**: hiki ni kipengele ambacho mwanafunzi anaposoma kwa ufasaha anapaswa kuhakikisha kwamba amethibiti kasi yake ya usomaji ili kusaidia ufahamu wa anachosoma. Kwa mujibu wa mtaala, kuna idadi ya maneno ambayo mwanafunzi anapaswa kusoma kwa dakika. Mwalimu anapaswa kumwelekeza mwanafunzi. kulingana na matokeo maalum kwenye mtaala. Wanafunzi wanaozidi matarajio wanaweza kusoma idadi zaidi ya maneno kwa dakika kama inavyoelekezwa na mtaala.

- **Matamshi bora:** msomaji anapaswa kuhakiksha kuwa anatamka maneno jinsi yanapaswa. matashi bora katika usomaji yanasaidia kufahamu matani inayosomwa. mwalimu anastahili kuhakikisha kuwa matamshi katika usomaji yanazingatikwa kikamilifu.

- **Kiimbo:** Kiimbo ni kupanda au kushuka kwa sauti. Katika usomaji wa matini, kuna maneno ambayo huwa na maana tofauti kulingana na kule kupanda au kushuka kwa sauti. mwanafunzi anaposoma matini maneno yanayohitaji kuwa na maana tofauti kwa mujibu wa kiimbo, anapaswa kuhakikisha kuwa yamezingatiwa. kushuka kwenyewe kunaweza kuwa katika silabi, sentensi au katika fungu. kwa mfano; *"Baba amefika" na "Baba amefika?"* sentensi hizi mbili zina maana tofauti kutegemea na jinsi ambavyo mwanafunzi anavyosoma. Maneno haya "*barabara"* na " *barabara*". maneno haya mawili yana maana mbili kutegemea na jinsi ambavyo msomaji anavyosoma.

- **Matumizi ya ishara:** Msomaji wa matini anapaswa pia kuhakikisha kuwa kama kuna ishara ambazo zinahitajika katika mchakato wa kusoma, msomaji sharti ahakikishe kuwa anazingatia ili aweze kuwasilisha ujumbe. kuna usomaji ambao unasisimua endapo anayesoma anahakikisha kuwa mahala kunahitaji ishara zimeingizwa na msomaji. ishara zinapotumiwa kikamilifu katika usomaji humnata msikilizaji kikamilifu na pia msikilizaji uweza kupata habari kikamilifu. Hadithi ambayo msomaji alisoma kwa kuzingatia ishara zifaazo katika maisha yako sharti hata leo unaikumbuka.